صَوْمُ يَوْمِ عَرَفَةَ

FUNGA YA SIKU YA ARAFA

⇒ JE KUNA MAFUNGAMANO BAINA YA SAUMU YA ARAFA NA KISIMAMO CHA ARAFA?

⇒ JE WATU KUFUATA MAKKA KATIKA SAUMU YA ARAFA NI UWAHABI?

⇒ JE KABLA YA KUWEPO REDIO, TELEVISHENI NA SIMU, VIPI WATU WAKIPEANA TAARIFA ZA MWEZI HAPA NCHINI, NA JE SASA WANAFUNGAJE?!

Mwandishi:

Abu Halima Arafaat Bin Mahmoud

NUKTA YA KWANZA

JE KUNA MAFUNGAMANO BAINA YA SAUMU YA ARAFA NA KISIMAMO CHA SIKU YA ARAFA?

Kuna baadhi ya Masheikh na wale wanaojifanya Masheikh wanajaribu kukata mawasiliano na mafungamano yaliyopo baina ya Saumu ya siku ya ARAFA na kisimamo cha ARAFA, kwa hoja kwamba jambo hili limekuja juzi tu, baada ya kupatikana vyombo vya mawasiliano, Redio, Televisheni, Simu n.k, je kabla ya vitu hivi wazee wetu wakifungaje?

Ufafanuzi: Kwanza hii si hoja ya kieleimu kabisa, kwa sababu miongoni mwa utaratibu wa sheria ya kiislamu ni: **kusilihi (kufaa) katika kila wakati na kila mahali** (haipitwi na wakati).

Mfano: leo hii kuna Nchi inaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kabla ya miaka Mia Moja jina hili halikuwepo, lakini watu walikuwepo na miji ilikuwepo; Tanga, Lindi, Mtwara, Rukwa, Songea, Dar es salaam n.k, wakati huo wala haikuwepo hiyo Redio Tanzania Dar es salaam (RTD). Je kabla watu wa Miji hii walikuwa wanafungaje? Mfano mwezi umeonekana Unguja je watu wa Kigoma watajuaje, au Tanga je watu wa Mtwara watafungaje? Je ikiwafikiaje habari ya mwezi mwandamo wa mji ulio mbali na wao kwa masafa ya kupunguza swala? Na je kwa sasa wanafungaje? Hii ni alama ya kwamba sheria ya kiislamu, kuna hali fulani zikijitokeza kuna mambo yanabadilika.

Imamu Ibn Taymiyyah رَحِمَهُ اللَّهُ ana maneno mazuri kuhusiana na jambo hili, wakati akifafanua kauli ya kwamba kila watu wa Miji wana mwezi wao, akasema:

وَالَّذِينَ قَالُوا: لَا تَكُونُ رُؤْيَةً لِجَمِيعِهَا كَأَكْثَرِ أَصْحَابِ الشَّافِعِيِّ مِنْهُمْ مَنْ حَدَّدَ ذَلِكَ بِمَسَافَةِ الْقَصْرِ وَمِنْهُمْ مَنْ حَدَّدَ ذَلِكَ بِمَا تَخْتَلِفُ فِيهِ الْمَطَالِعُ: كَالْحِجَازِ مَعَ الشَّامِ وَالْعِرَاقِ مَعَ خُرَاسَانَ وَكِلَاهُمَا ضَعِيفٌ؛ فَإِنَّ مَسَافَةَ الْقَصْرِ لَا تَعَلُّقَ لَهَا بِالْهِلَالِ. وَأَمَّا الْأَقَالِيمُ فَمَا حَدَّدَ ذَلِكَ؟

“Na wale ambao wanasema, haiwezekani kuwa kuona mwezi ni kwa watu wote, kama walivyokuwa wengi katika wafuasi wa (imam) Shaf’i, kuna miongoni mwao walioweka mpaka wa hilo kwa masafa ya kupunguza swala, na kuna walioweka mipaka ya hilo kwa kutafautiana matwaali’ (machimbuko ya jua), kama vile Hijaaz[1] pamoja na Sham[2], na Iraq pamoja na Khuraasan[3], na kauli zote hizo ni dhaifu , kwa sababu masafa ya kupunguza swala hayana mafungamano yoyote na mwezi mwandamo, na ama kuzingatia majimbo ni upi mpaka wa hilo?”.

Maana yake ni kwamba ukisafiri kwenda mji mwingine kwa umbali wa masafa ambayo unaruhusiwa wewe kupunguza swala, basi mwezi wa watu wa mji huo ni tafauti na mwezi ule wa mji uliotoka (huo ni mwezi wao). Kadhaalika majimbo, ni kutoka jimbo gani mpaka jimbo gani?

Imamu Ibn Taymiyyah رَحِمَهُ اللَّهُ ameitia makosa misimamo hiyo kwa njia mbili, akaitaja njia ya pili akasema:

الْوَجْهُ الثَّانِي: "أَنَّهُ إذَا اعْتَبَرْنَا حَدًّا: كَمَسَافَةِ الْقَصْرِ أَوْ الْأَقَالِيمَ فَكَانَ رَجُلٌ فِي آخِرِ الْمَسَافَةِ وَالْإِقْلِيمِ فَعَلَيْهِ أَنْ يَصُومَ وَيُفْطِرَ وَيَنْسُكَ وَآخَرُ بَيْنَهُ وَبَيْنَهُ غَلْوَةُ سَهْمٍ لَا يَفْعَلُ شَيْئًا مِنْ ذَلِكَ وَهَذَا لَيْسَ مِنْ دِينِ الْمُسْلِمِينَ"

“Njia ya pili: ni kwamba tukizingatia mpaka wa masafa ya kupunguza swala au mpaka wa majimbo, kisha mtu akawa yuko katika masafa ya mwisho ya kupunguza swala au mwisho wa jimbo, basi ni wajibu juu yake kufunga na kufungua, au kufanya Hija (au ibada ya kuchinja), na mwingine kuna baina yake na baina ya hilo jimbo kiasi cha kutupa mkuki tu hatafanya chochote katika hayo, na hii sio Dini ya waislamu”[4].

Maana yake, mfano mtu akiwa mpakani mwa Tanzania na Kenya (Horohoro), mwezi ukionekana Tanga atafunga kwa sababu ni katika nchi, lakini mtu aliyopo Lungalunga (upande wa Kenya) ataukataa mwezi huo kwa sababu tu ya mipaka, wakati akitupa mkuki utafika upande wa

---

1- Neno Hijaaz linakusanya: (Makka, Madina na viunga vyake).
2- Na Sham inakunya: Syria, Palestina, Lebanon na Jordan.
3- Khuraasan kwa sasa inapatikana kusini maghrib mwa Nchi ya Afghanistan.
4- Angali: [Majmul Fataawa] (Jz. 25, Uk. 104 - 106).

Tanzania, na kinyume chake ataukubali mwezi ulioonekana Garisa, pamoja masafa ya kutoka Lungalunga mpaka Tanga ni karibu kuliko kutoka Lungalunga kwenda Garisa.

Ndio maana Ibn Taymiyyah رَحِمَهُ اللهُ akasema

"وَالِاعْتِبَارُ بِبُلُوغِ الْعِلْمِ بِالرُّؤْيَةِ فِي وَقْتٍ يُفِيدُ"

"Mazingatio yapo katika kufika elimu ya kuonekana mwezi katika wakati unaotoa faida"[5].

Hili ndio jawabu la yule anaesema kwamba, watu kufunga pamoja na watu wa Makka au kufunga sawa na siku waliosimama mahujaji katika viwanja vya Arafaat, jambo hili limekuja juzi tu. Basi pia afahamu hata mtu wa Mtwara kujua kwamba hivi sasa Mufti wa Zanzibar anatangaza kuwa mwezi umeoneka Makunduchi, hali hii imekuja juzi tuu, kadhaalika mtu wa kigoma kujua kwamba Mufti wa Tanzania anaeishi Dar, hivi sasa anatangaza kuwa mwezi umeonekana Bagamoyo, imekuja juzi tuu.

Swali: Je kabla ya kuwepo vitu hivi (redio, simu, televisheni), vipi wakifunga na kufungua katika Ramadhani, kadhaalika saumu ya siku ya Arafa? Ukisema kabla ya redio kila watu walikuwa na mwezi wao, basi tunaomba utupe faida, kwanini leo watu wote (Zanzibar, Kilwa, Kigoma, Mtwara, Musoma n.k) wanafunga pamoja, kitu gani kimewaondoa kwenye ile hali waliokuwa nayo hapo mwanzo ya kila watu kufunga na mwezi wao kama si kupatikana vyombo vya mawasiliano?!

Ikiwa jawabu ni ndio, basi ndio maana leo kuna wepesi watu wote kufunga siku ileile ambayo mahujaji wamesimama katika viwanja vya Arafaat, kwa sababu ya kuwepo vyombo vya mawasiliano ya haraka, kama alivyosema Ibn Taymiyyah: **"Mazingatio yapo katika kufika elimu ya kuonekana mwezi katika wakati unaotoa faida".** Na wale wanaohoji, vipi watu walio mashariki ya mbali? Tutamwambia wao wana hukumu yao na wewe una hukumu yako.

---

[5]- Angali: [Majmul Fataawa] (Jz. 25, Uk. 106).

Nini maana ya wakati unaotoa faida?

Maana yake ni kwamba taarifa imekufikia wewe katika wakati ambao unaweza kufunga na ikasihi saumu yako (kama vile kupata taarifa usiku kabla kuchomoza alfairi ya kweli), lakini mfano: taarifa imekufikia leo kwamba jana mwezi ulionekana huko Mbeya, wakati huo itasemwa kwamba taarifa hii haijakupatia wewe faida yoyote, bali hapo tutaifanyia ile hadithi ya Kuraib رَحِمَهُ اللَّهُ kama wanavyoeleza Maulamaa.

Ndio maana Ibn Taymiyyah رَحِمَهُ اللَّهُ akasema:

"فَأَمَّا إِذَا بَلَغَتْهُمْ الرُّؤْيَةُ بَعْدَ غُرُوبِ الشَّمْسِ فَالْمُسْتَقْبَلَ يَجِبُ صَوْمُهُ بِكُلِّ حَالٍ لَكِنَّ الْيَوْمَ الْمَاضِيَ: هَلْ يَجِبُ قَضَاؤُهُ"

"Ama ikiwafikia wao habari ya kuonekana mwezi baada ya kuzama jua, basi (huo utakuwa ni mwezi wa siku) inayofuatana, kutapasa kuifunga hiyo siku inayofuata kwa hali yoyote, lakini ile siku iliyopita, je itafaa kuilipa?".

Kwa hiyo mazingatio ni kufikiwa na elimu kwamba mwezi umeonekana, na watu watasimama Arafa siku fulani.

Swali: Je hivi sasa kuna kizuizi gani kinachotuzuia sisi Watanzania na Afrika mashariki bali Duniani kote kupata taarifa kwamba leo siku ya Ijumaa mwaka huu (1443H – 8/7/2022) Mahujaji watasimama Arafa?.

Ama hoja ya watu waliopo mbali kiasi ambacho wao hivi sasa ni usiku, pia haina nguvu yoyote, yatakuja majibu yake kwenye Makala zijazo In Shaa Allaah, lakini tunajadili kuhusu wewe uliye karibu, sasa usitake kulinganisha hukumu yako wewe na huyo aliye mbali, kama vile mwenye wa ramadhani, mtu aliye katika mji (mkazi) hukumu yake ni tafauti na msafiri, dereva n.k. kwa hiyo kila kitu kiwekwe mahali pake.

Alhamdulillah, hapa nitakuwa nimeikamilisha Nukta ya kwanza.

Wabillahi Ttaufiiq

NUKTA YA PILI:
Je Watu Kufuata Makka Katika Saumu ya Arafa Ni Uwahabi?

Hapa tutanukuu maneno ya mmoja miongoni mwa masheikh wa Twariqa ya Qadiriyya hapa nchini akiitwa sheikh Muhammad Nassor Abdulla El-Qadiry, katika [KITABU AFARA] Uk. 5-6 kwa namba za kirumi (v-vi):

KITABU ARAFA
NGUZO KUBWA YA HIJJA NDIO ARAFA TAREHE TISA MFUNGO TATU NA KUSWALI IDD EL-HAJJ SAWA NA MAKKA

Amesema: "Madhumuni haswa ni kufafanua mgogoro/tatizo lililopo hapa nchini kuhusu Arafa. Baadhi ya watu hapa nchini mpaka sasa wanafunga siku ya Arafa ya Makka kwa kufuata tarehe 9 Mfungo tatu ya mwezi wa hapa kama ilivyokuwa huko nyuma wakati ambao hakukuwa na mawasiliano kati yetu na Makka. Kwa wakati ule ilikuwa ni sawa kufanya Ibada kwa mwezi wetu, kwani ilikuwa Ibada ya Jitihada".

Akasema tena katika Uk. 25: "Kwa maneno ya Hadithi hii, hivyo dunia nzima pia Waislamu wote tunatakiwa kufunga Arafa katika siku hii hii ya Arafa ya Makka iliyotangazwa na Imamu wa Makka, na sio kila mtu awe na Arafa yake mwenyewe".

Akaendelea akasema: "Inasikitisha kuona kwamba ni sisi tu hapa nchini kwetu ndiyo bado hatujazindukana katika kutambua ukweli huu. Waislamu hivi sasa wa dunia nzima wanafunga Arafa kwa kufuatana na Arafa ya Makka. Wapo baadhi tu ya Waislamu hapa nchini kwetu wasiofuata Arafa ya Makka, Wanasema kwamba Ibada za Hijja kwa sisi tusiokwenda kuhiji Makka hazituhusu. Wanasema Ibada hizo zinawahusu Mahujaji tu peke yao huko Makka. Na ndio maana kwa hoja yao hii wao hufunga Arafa kwa siku waitakayo wao. Hayo ni makosa makubwa".

Hizi ni jumla ya faida kutoka kwenye Darsa za Sheikh Abul Fadhli حَفِظَهُ اللَّهُ

Abu Halima Arafaat
Ijumaa/siku ya Arafa 09/Dhul-hijja/1443H – 08/07/2022M
Pongwe Tanga.